TRC
SHIRIKA LA RELI TANZANIA

# RELI na MATUKIO

*Gazeti*

Aprili 03, 2021




Gazeti la Reli | Toleo Namba 13 | Habari | Makala | Matukio | Elimu | Picha

# TRC YAOMBOLEZA KIFO CHA DKT. MAGUFULI




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan akiweka shada la maua juu ya kaburi la aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli wakati wa shughuli za mazishi Chato mkoani Geita, Machi 2021.







# TRC YAOMBOLEZA KIFO CHA DKT. MAGUFULI

Na Mwandishi wetu TRC



Mjane wa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mama Janeth Magufuli akiweka shada la maua katika kaburi la marehemu wakati wa maziko hayo yaliyofanyika Chato Mkoani Geita Machi, 2021.




Watoto wa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakiweka Shada la Maua katika kaburi la baba yao wakati wa maziko yaliyofanyika Chato Mkoa wa Geita Machi, 2021.




Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa akitoa heshima za mwisho kwa mwili wa Hayati Dkt. John Pombe Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam Machi 2021.

Shirika la Reli Tanzania – TRC limeungana na Watanzania wote katika siku 21 za maombolezo kufuatia kifo cha aliyekuwa Rais wa Awamu ya Tano ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli kilichotokea Machi 17, 2021.

Aidha, uongozi na wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania wakiwakilishwa na Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa wameshiriki katika shughuli za kuaga na kutoa heshima za mwisho pamoja na mazishi ya Hayati Dkt. Magufuli.

Shirika la Reli Tanzania litamkumbuka Hayati Dkt. Magufuli ambaye ni Muasisi wa utekelezaji wa Mradi Mkubwa wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR nchini, halikadhalika Dkt. Magufuli aliweza kufanya jitihada nyingi kuhakikisha Shirika linaimarika kwa kuliwezesha kutoa huduma kwa ufanisi kupitia ukarabati wa reli ya kati kutoka Dar es Salaam hadi Isaka, ukarabati wa Behewa 200 za mizigo, Ukarabati wa Vichwa Sogeza 7 vya treni, ununuzi wa vichwa vipya 11 vya Treni na ufufuaji wa reli ya Kaskazini (Tanga - Moshi - Arusha) na hatimaye huduma kurejea.

Sambamba na hayo yote Dkt. Magufuli kupitia uongozi wake aliweza kuwajengea watumishi hali ya kujituma na kuwajibika hivyo kuliwezesha Shirika kuwa miongoni mwa mashirika yanayoaminika katika utoaji huduma.

Katika moja ya Hotuba za Hayati Dkt. Magufuli aliwahi kusema kuwa "Nataka Shirika hili liwe mfano Afrika kwa kuhudumia wananchi wake wakiwemo wanyonge na kufanya biashara, wito wangu kwenu hakikisheni mnafanya kazi na gharama zenu zinakuwa za chini"

Shirika litamuenzi hayati Dkt. Magufuli kwa kuchapa kazi kwa kutoa huduma bora na za uhakika za usafiri wa abiria na usafirishaji wa Mizigo na kusimamia vyema miradi ya shirika kwa maslahi ya watanzania ili kufikia Maono ya Dkt. Magufuli ya kulifanya Shirika la Reli kuwa mfano barani Afrika kwa kuhudumia wananchi.

# HONGERA

**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN**
**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



**Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika la Reli Tanzania - TRC wanampongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# SGR SASA NI MWANZA - ISAKA, MKATABA WA MRADI WA SGR WASAINIWA



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kadogosa (kulia) na Muwakilishi wa Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation na China Railway Construction Corporation Limited (CRCC) Bwana Zhang Junle wakitiliana saini mkataba wa ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kutoka Mwanza hadi Isaka, Chato mkoani Geita Januari 2021.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imetia saini mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa kwa kipande cha tano Mwanza – Isaka. Mkataba umesainiwa kati ya TRC na ubia wa kampuni mbili za Kichina 'China Civil Engineering Construction Corporation (CCECC) na China Railway Construction Corporation Limited (CRCC)' Januari 2021.

Ujenzi wa Reli ya kisasa awamu ya kwanza ni Dar es salaam - Mwanza wenye jumla ya kilomita 1219 ambao umegawanyika katika vipande vitano (5). Kipande cha kwanza Dar es salaam - Morogoro kilomita 300, kipande cha pili Morogoro - Makutupora kilomita 422, kipande cha tatu Makutupora - Tabora Kilomita 371, kipande cha nne Tabora – Isaka kilomita 162 na kipande cha tano ni Isaka-Mwanza kilomita 341.

Inaendelea Uk. 4

# MKATABA WA MRADI WA SGR MWANZA ISAKA WASAINIWA

Na Mwandishi wetu TRC Inatoka Uk 3



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania - TRC Ndugu Masanja Kadogosa (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation na China Railway Construction Corporation Limited (CRCC) Bwana Zhang Junle wakionesha nakala za mkataba wa ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR kutoka Mwanza hadi Isaka mara baada ya kutiliana saini, Chato mkoani Geita Januari 2021.

Awamu ya kwanza ya ujenzi huo kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro yenye kilometa 300, imefikia asilimia 90, huku awamu ya pili ya Morogoro hadi Dodoma yenye kilometa 422, ujenzi wake ulioanza mwaka jana sasa umefikia zaidi ya asilimia 52.

Mkataba uliosaniwa ni wa miezi thelathini na sita (36) na thamani ya mradi ni shilingi za kitanzania trilioni 3.0617 pamoja na kodi. Fursa zitakazopatikana ni ajira na malighafi za ujenzi ambapo ajira moja kwa moja ni 15,000 na zisizo za moja kwa moja ni 75,000 na malighafi za ujenzi ni saruji na nondo na saruji itakayotumika inakadiriwa kuwa kiasi cha mifuko 2,500,000.

Akizungumzia zabuni hiyo, Hayati Dkt. John Magufuli akiwa kwenye kampeni mkoani Simiyu, alieleza kuwa baada ya kupatikana mzabuni kupitia tangazo, ujenzi utaanza mara moja kwa kuwa fedha zipo.

“Wiki iliyopita tumetangaza zabuni kutoka Mwanza-Malampaka-Shinyanga mpaka Isaka. Mkandarasi akipatikana anaanza kutengeneza hiyo awamu, fedha ipo na wataalamu wapo,” alisisitiza Hayati Dkt, Magufuli aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema kwa sasa sekta ya reli inaendelea vizuri na Mkurugenzi Mkuu wa TRC, Masanja Kadogosa pamoja na watalaamu, waliwezesha mradi huo wa SGR kuanza na sasa unaendelea vizuri.

“Nilimwambia Kadogosa tuanze kujenga reli ya umeme kama nchi za wenzetu, nikamuambia kakae na wataalamu wenzako. Nyie ni mashahidi miundombinu ya ujenzi wa reli ya umeme Dar es Salaam inaonekana inapita juu zaidi ya kilometa 20 na ndani ya mahandaki Morogoro zaidi ya kilometa tano,” alisema.

Alisema awamu ya pili ya SGR kutoka Morogoro kwenda Dodoma, inaendelea vizuri na fedha zitakazotumika katika ujenzi huo Sh trilioni 7.62 zipo.

“Nawaomba vijana na mama lishe huu ndio wakati wa kutajirika. Kupitia reli kutoka Dar es Salaam hadi Kigoma tumeajiri watu zaidi ya 10,000. Hapa napo kupitia SGR tutaajiri maelfu ya Watanzania,” alieleza.

Awamu ya kwanza ya SGR ilianza kujengwa Mei 2, mwaka 2017 na hadi kukamilika kwake itagharimu zaidi ya Sh Trilioni mbili.

Reli hiyo SGR ina uwezo wa kubeba tani milioni 10,000 kwa mkupuo, sawa na malori 500 yenye tani 20, treni tano zenye tani 10,000. Treni hiyo itakuwa na kasi ya kilometa 160 kwa saa tofauti na ya sasa ambayo ina kasi ya kilometa 30 kwa saa.

# WAZIRI MKUU; RAIS MAGUFULI ALIAMUA KUBORESHA MIUNDOMBINU NCHINI

Na Mwandishi wetu TRC

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa amesema Hayati Rais Dkt. John Pombe Magufuli aliamua kuboresha miundombinu mbalimbali ya usafiri nchini ikiwemo ujenzi wa mradi wa reli ya kisasa (SGR) ili kurahisisha usafirishaji wa abiria na mizigo.

Ameyasema hayo Machi 5, 2021 akiwa jijini Dodoma kukagua maendeleo ya sehemu ya kipande cha pili cha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa cha kutoka Morogoro hadi Makutupora mkoani Singida.

Waziri Mkuu amesema ameridhishwa na kazi nzuri inayoendelea kufanywa na amewataka wananchi wajiandae kutumia reli hiyo ambayo inajengwa kwa ajili yao. Amesema kukamilika kwa mradi huo kutaongeza ufanisi wa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kupunguza muda wa safari, mfano kutoka Dar es Salaam – Dodoma muda utakuwa saa tatu badala ya saa nane za sasa.

Waziri Mkuu amewataka Watanzania waliopata kazi katika mradi huo wafanye kazi kwa uaminifu na weledi wa hali ya juu ili kuudhihirishia ulimwengu kwamba Watanzania wanaajirika. “Endeleeni kuchapakazi nyinyi ni mabalozi mtakaowawezesha wengine kupata ajira.”

Aidha, Waziri Mkuu amewataka Watanzania wahakikishe wanazielewa vizuri shughuli wanazozifanya katika mradi huo ili baadaye waweze kuisimamia wenyewe reli hii ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati. “Tumieni ujenzi wa mradi huu kama sehemu ya kupata utaalamu”.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Ndugu Masanja Kadogosa amesema ujenzi wa kipande cha pili cha mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Morogoro hadi Makutupora umefikia asilimia 56.1 na unatarajiwa kukamilika Februari, 2022.

Amesema kukamilika kwa mradi huo kutashusha gharama za usafirishaji mizigo kati ya asilimia 30 mpaka 40 na kuifanya bandari ya Dar es salaam kuhimili ushindani. Kipande cha kutoka Morogoro – Makutupora chenye urefu wa kilomita 422 kinajengwa na Kampuni ya Yapi Merkezi kutoka nchi ya Uturuki kwa gharama ya shilingi bilioni 4.4.

“Reli hii itachochea mapinduzi ya kiuchumi kwa kanda nzima ya Afrika Mashariki na Kati hususani nchi zisizopakana na Bahari, hivyo kuchangia katika kukuza uchumi wa Taifa. Pia mradi huu utachochea uanzishwaji wa viwanda katika maeneo mengine ya nchi kwa kuwa utoa uhakika wa usafirishaji wa mali ghafi na bidhaa.”

Kadogosa amesema mpaka kufika tarehe 01 Machi, 2021 mradi huu ulikuwa na wafanyakazi 8,014, ambapo 6,472 sawa na asilimia 81% ni Watanzania na 1,542 sawa na asilimia 19% ni raia wa kigeni na kwamba TRC imeendelea kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wataalamu wake mbalimbali, ambapo kwa sasa zaidi ya wataalamu 40 wanashiriki moja kwa moja kwenye ujenzi wa mradi wa SGR.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa akikagua ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR), inayojengwa na Kampuni ya Yapi Markezi, wakati alipokagua maendeleo ya ujenzi wa kipande cha Ihumwa- Igandu ikiwa ni sehemu ya pili ya mradi huo, kutoka Morogoro hadi Makutupora mkoani Dodoma, Machi, 2021

# KAMATI YA BUNGE YA MIUNDOMBINU YAKAGUA MRADI WA SGR NA KARAKANA



Na Mwandishi wetu TRC

Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Miundombinu yakagua Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa Dar es Salaam - Makutupora na Karakana ya reli mkoani Morogoro, ziara hiyo imefanyika kuanzia Machi 12 - 13, 2021.

Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya miundombinu pamoja na kuweka mikakati ya kutetea bajeti ya miundombinu katika bunge la bajeti linalotarajiwa kuanza hivi karibuni.

Aidha, kamati imeridhishwa na utendaji wa Shirika hususani katika usimamizi wa miradi ukiwemo mradi wa SGR kutoka Dar es Salaam hadi Makutupora ambapo kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro ujenzi wake umefika zaidi ya 90% ukitarajiwa kukamilika Agosti 2021 na kipande cha Morogoro - Makutupora ambacho ujenzi wake umefika 56%, halikadhalika mradi wa ukarabati wa vichwa sogeza 7 ambavyo vimekamilika tayari kwa ajili ya kuanza kazi.

Aidha, Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa amesema kuwa lengo la ziara hiyo ni kwa ajili ya kuona maendeleo ya mradi sambamba na matumizi ya pesa ambazo zilipitishwa na bunge ili kutekeleza mradi huo.

"Wizara yetu inahusika kiutendaji na bajeti ya miundombinu, leo tumepata ugeni huu tunashukuru kwa sababu hiki ni kipindi cha bajeti hivyo wanapokuja wanapata fursa ya kuona matumizi ya pesa walizopitisha katika bunge la bajeti lililopita na kuendelea kutetea bajeti ili kuendelea kutekeleza mradi huu" alisema Kadogosa

Mkurugenzi ameongeza kuwa bado Shirika linaendelea kusisitiza ushiriki wa wazawa katika mradi ambapo kwa hivi sasa katika kazi nyingi zinazoendelea wanaofanya na kusimamia kazi hizo ni wazawa, mfano mzuri ni katika kiwanda cha Mataruma ambacho wajumbe wameweza kujionea kuwa wafanyakazi wote wanaosimamia kiwanda hiko ni watanzania.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu Mhe. Selemani Kakoso ametoa Shukurani zake kwa Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali kwa kazi kubwa kwa kuwa kazi katika kipande cha Dodoma – Morogoro kinakwenda vizuri na kuongeza kuwa wanakamati wana imani kuwa fedha wanazoidhinisha Bungeni zinafanya kazi kwa ajili ya manufaa ya taifa.

Mhandisi Mwanaisha Ulenge, Mbunge wa Viti Maalumu mkoa wa Tanga na Mjumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu amepongeza Shirika la Reli kwa usimamizi mzuri wa mradi huo kwa kuzingatia viwango pamoja na utendaji wa kazi za ujenzi katika mradi huo.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa akiwapatia maelezo wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu ujenzi wa jengo la Stesheni ya SGR jijini Dar es Salaam hivi karibuni Machi, 2021.



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kadogosa akiwapatia maelezo wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu ujenzi wa jengo la Stesheni ya SGR jijini Dodoma, hivi karibuni Machi, 2021.

Na Mpiga Picha wetu TRC



Muonekano wa Sehemu wa jengo la Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR jijini Dar es Salaam nyakati za Usiku, likiwa limekamilika kwa 100%.



Muonekano wa Sehemu wa jengo la Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR mkoani Morogoro likiwa limekamilika kwa 100%.




Vichwa Sogeza 7 vya Treni vikiwa vimekamilika na vinatarajiwa kuanza kazi hivi karibuni ili kuongeza ufanisi wa Shirika katika ubebaji Mizigo.



Sehemu ya kukata na kupata taarifa za Tiketi ndani ya jengo la Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR jijini Dar es Salaam.



Sehemu ya kukata na kupata taarifa za Tiketi ndani ya jengo la Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR mkoani Morogoro.



Mgahawa wa Watu Maalumu (VIP) ndani ya jengo la Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR ukiwa na muonekano mzuri wa jiji la Dar es Salaam.



Mgahawa wa Watu Maalumu (VIP) ndani ya jengo la Stesheni ya Reli ya Kisasa - SGR mkoani Morogoro.

# TRC YAIBUKA KIDEDEA KWA KUPATA TUZO YA KURASA BORA YA SERIKALI MTANDAONI



Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la Reli Tanzania laibuka kidedea kwa kupata tuzo ya kurasa bora ya serikali mtandaoni iliyopokelewa kwenye hafla fupi iliyoandaliwa na uongozi wa Shirika la Reli Tanzania - TRC katika ukumbi wa Akemi hivi karibuni Februari, 2021.

TRC imeshinda Tuzo hiyo baada ya kushindanishwa katika kipengele cha Kurasa Bora ya Serikali Mtandaoni inayohabarisha wananchi ambapo mashindano hayo yaliyoandaliwa na kampuni ya Serengeti Bytes kwa kushirikisha mashirika na taasisi zote za Serikali.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa amesema kuwa tuzo hiyo ni kubwa kwa Shirika na inadhihirisha kuwa kinachofanyika katika shirika la reli wananchi wengi wanaona kupitia taarifa zake na kinaleta manufaa katika nchi.

“Sisi tumeona ni jambo kubwa na hata katiba yetu ya Taifa inatambua vitu vinavyofanyika ndani ya Serikali lazima watu wawe na taarifa“ aliongezea kuwa “Tunatimiza suala la kisheria na vilevile tunatendea haki watanzania wajue pesa yao ya kodi inakwenda wapi” alisema Ndugu Kadogosa.

Pia Ndugu Kadogosa alieleza kuwa ushindi huo umeleta matokeo kwa wananchi na kuwa watu zaidi ya milioni saba wanaona na wanahabarika kupitia mtandao wa TRC Reli TV wa Youtube na pia kupitia mitandao mengine na Instagram, Twitter, Facebook na Tovuti ya TRC.

Naye Mkurugenzi Mtendaji katika kampuni ya Serengeti Bite Bw. Michael malya amesema kuwa TRC ilishindana kama kipengele cha serikali mtandaoni na wameibuka kidedea baada ya kupata kura nyingi kutoka kwa wananchi. “TRC ilipigiwa kura kama Taasisi bora ya Serikali ambayo inafanya matumizi bora ya mtandao ya kijamii katika kufikia umma” alisema Bw. Malya.

Aidha Bw. Malya ameipongeza sana TRC na kusema kuwa TRC imetoa hamasa kwa taasisi nyingine za Serikali kujifunza na kuendelea kuboresha kwa kufanya kazi nzuri kupitia majukwaa ya mitandao ambayo wananchi wengi wanaona kazi zinazoendelea kiurahisi zaidi.

“Lengo la Tuzo za kidigitali ni kuongeza ubunifu katika matumizi ya teknolojia hasa za kidigitali na pia kuongeza uwajibikaji katika Taasisi” aliongezea Bw. Malya.

Mkuu wa Kitengo cha Habari TRC Bi. Jamila Mbarouk alisema kuwa kupitia tuzo hiyo TRC imezidi kupata nguvu mpya na faraja ya kufanya vyema zaidi katika kuhabarisha umma kwa njia ya mtandao kupitia kitengo cha habari cha shirika. “TRC tumeweza kujikita katika upashaji wa habari na tunatumia kujitangaza katika njia mbalimbali za mtandao” alisema Bi. Jamila.

Bi. Jamila ametoa shukurani za dhati kwa Mkurugenzi Mkuu, menejimenti na wafanyakazi wote wa TRC kwa kutoa ushirikiano mzuri kwa kitengo cha habari na kukipa nguvu za kuweza kufanya kazi kwa ufanisi, pia alitoa shukurani kwa timu ya kitengo cha habari kwa kujitoa katika kazi pamoja na ubunifu ambao umeleta heshima kubwa TRC.




Mkurugenzi Mkuu TRC Ndugu Masanja Kadogosa (wa pili kulia) akipokea tuzo ya Kurasa Bora ya Serikali Mtandaoni kutoka kwa waandaaji wa tuzo hizo Kampuni ya Serengeti Bytes katika ukumbi wa Akemi jijini Dar es Salaam hivi karibuni Februari, 2021.

# TRC IMEKABIDHI BEHEWA 40 KWA SHIRIKA LA MPANGO WA CHAKULA DUNIANI - WFP



Na Mwandishi wetu TRC



Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Godfrey Kasekenya (wa pili kulia) akikata utepe kuashiria makabidhiano ya behewa 40 kati ya TRC na WFP katika kituo cha mizigo Ilala jijini Dar es Salaam hivi karibuni Februari 2021

Shirika la Reli Tanzania – TRC limekabidhi behewa 40 za mizigo kwa Shirika la mpango wa chakula duniani - WFP katika hafla fupi iliyofanyika katika kituo cha mizigo Ilala jijini Dar es Salaam hivi karibuni Februari 2021.

Hafla hiyo imehudhuriwa na viongozi mbalimbali wa Serikali wakiwemo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Godfrey Kasekenya ,Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Profesa John Kondoro, Mkurugenzi Mkuu TRC Ndugu Masanja Kadogosa, Mkurugenzi Mkazi - WFP Bi. Sarah Gordon, Uongozi wa Shirika la Reli Tanzania, Wafanyakazi TRC Wawakilishi kutoka Shirika la Mpango wa Chakula Duniani - WFP Wadau wa TRC na WFP, Pamoja na Wanahabari.

Lengo la kukarabati mabehewa 40 ni Kudumisha uhusiano wa kibiashara uliodumu kwa muda mrefu kati ya TRC na WFP na Kuongeza uwezo wa usafirishaji mizigo ya WFP kwa njia ya reli na kuifanya sekta ya reli kuwa kichochea katika ukuaji wa uchumi wa Nchi na kupelekea Tanzania kuendelea kufanya vizuri kiuchumi.

Aidha Shirika la Reli Nchini limekuwa na ushirikiano na baadhi ya wadau mbalimbali wakiwemo Shirika la chakula Duniani (WFP), wadau hao wameshiriki kikamilifu kwa kufanya ukarabati wa behewa ambazo hutumika katika kusafirisha mizigo yao lakini pia hutumika kuhudumia mizigo ya wasafirishaji wengine jambo ambalo limesaidia kuongeza ufanisi wenye tija kwa kwa Shirika la Reli katika kuhudumia mizigo hususani inayotoka katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mgeni Rasmi Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Godfrey Kasekenya, ameishukuru Serikali ya awamu ya tano kwa kuendelea kuunga mkono jitihada zinazofanywa na Shirika la reli pamoja na wadau katika kuimalisha sekta ya reli kwa kukarabati behewa ili kuongeza ufanisi katika kuhuma za usafirishaji wa mizigo.

“Naishukuru Serikali ya awamu ya tano ilipo ingia madarakani ilijikita kuinua Shirika la reli nchini ambapo ilitoa kiasi cha Shilingi Bilioni 4 (nne) za kitanzania kwa ajili ya kukarabati behewa 200, ambapo kwa sasa nimetaarifiwa jumla ya mabehewa 162 yameshakarabatiwa na behewa 38 zinaendelea kwa ukarabati” alisema Naibu Waziri.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TRC Prof. John Kondoro, alibainisha uhusiano uliopo kati ya TRC na WFP kuwa ni maagizo ya Wizara yenye dhamana katika kuhakikisha Serikali kwa kushirikiana na Shirika inashirikisha wadau mbalimbali na wafanyabishara.

Inaendelea Uk. 10

# TRC IMEKABIDHI BEHEWA 40 KWA SHIRIKA LA MPANGO WA CHAKULA DUNIANI - WFP

Na Mwandishi wetu TRC Inatoka Uk. 9




Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Godfrey Kasekenya akipeperusha bendera kuruhusu treni yenye Behewa zilizokarabatiwa kwa ushirikiano kati ya TRC na WFP katika hafla ya kukabidhi Behewa hizo katika kituo cha mizigo Ilala jijini Dar es Salaam hivi karibuni Februari 2021




Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Godfrey Kasekenya (aliyeketi wa nne kulia) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti ya Bodi ya Wakurugenzi TRC, Prof. John Kondoro (aliyeketi wa tatu kulia), Uongozi wa TRC, WFP na baadhi ya wadau wakiwemo TPSF na Yapi Merkezi baada ya makabidhiano ya behewa 40 kati ya TRC na WFP katika kituo cha mizigo Ilala jijini Dar es Salaam hivi karibuni Februari 2021

"Ushirika huu ni utekelezaji wa melekezo ya Wizara tuweze kushirikisha wadau na wafanyabiasha ili tuweze kuimarisha shirika letu. Tunaendelea kushirikisha wadau wengine na huu ni mwanzo kwamba leo tunashuhudia makabidhiano ya behewa 40 ambazo zimegharamiwa na WFP tutaendelea kushirikisha wadau wengine kwa kuwa uhitaji wa mabehewa ni mkubwa sana" alisema Prof. Kondoro.

Naye Mkurugenzi Mkuu TRC, alitoa takwimu ya behewa zilizokamilika kukarabatiwa na zinazohitajika kukarabatiwa sambamba na kutoa wito kwa wadau wengine wa usafirishaji kuendelea kuunga mkono juhudi za Mhe. Rais John Pombe Magufuli za kuimarisha sekta ya reli nchini.

"Behewa zinazohitajika kufanyiwa ukarabati mkubwa ni 500, ambapo behewa 200 tayari zinagharamiwa na Serikali. Takribani behewa 300 zinahitaji kukarabatiwa, kutokana na hilo bado TRC inajukumu la kuboresha behewa hizo na tunaendelea kukaribisha wadau katika sekta mbalimbali tushirikiane kwa pamoja kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kukarabati behewa zilizobaki" alisema Mkurugenzi Mkuu.

Hata hivyo Mkurugenzi Mkazi - WFP Bi. Sarah Gordon alieleza namna WFP ilivyo shiriki kuinua uchumi wa usafirishaji nchini kupitia sekta ya reli ndani ya miaka miwili, ambapo alieleza pia maono ya ushirikiano huo utakavyoleta tija kiuchumi katika siku za mbeleni.

"Mwaka 2018 mpaka 2020 WFP ilinunua hapa nchini bidhaa za chakula tani za uzito 262,000 na kuiingizia uchumi wa nchi jumla ya dola za kimarekani milioni 160 kutokana na manunuzi pamoja na huduma ya usafirishaji wa tani hizo, nimatumaini yetu kwamba uhusiano huu wa kiabiasha utaendelea kukua hata kwa siku zijazo" alisema Bi. Sarah Gordon.

Ushirikiano uliopo kati ya wadau wa sekta ya reli nchini, wafanyabiashara pamoja na Shirika la reli Tanzania ni kiungo kikubwa katika kuleta maendeleo ya uchumi wa usafirishaji nchini ambapo WFP wameonesha nia na faida imeonekana kwa sasa na hata kwa siku zijazo katika kuongeza ufanisi wa utendaji kazi ndani na nje ya nchi.

# TRC NA TPSF WAFANYA KONGAMANO LA KWANZA LA WADAU KUJADILI FURSA KATIKA MRADI WA SGR

Na Mwandishi wetu TRC



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa akieleza fursa zilizopo katika mradi wa SGR katika Kongamano lilofanyika katika Ukumbi wa BOT jijini Mwanza hivi karibuni January 2021

Shirika la Reli Tanzania – TRC kwa kushirikiana na Taasisi ya Sekta Binafsi Nchini – TPSF wamefanya kongamano la kwanza la wadau wa sekta binafsi kujadili fursa katika mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa – SGR kipande cha Mwanza – Isaka katika ukumbi wa Benki Kuu ya Tanzania jijini Mwanza hivi karibuni Januari 2021.

Lengo la Kongamano hilo ni kuandaa mpangokazi wa ushirikishwaji wa Sekta binafsi nchini katika mradi huo unaotarajiwa kuanza utekelezaji wake hivi karibuni ambapo Mkandarasi kutoka China kampuni ya China Civil Engineering Construction Corporation pamoja na China Railway Construction Company watatekeleza mradi huo.
“Leo tumekutana hapa kujadili ujenzi wa reli ya kisasa na jinsi tutakavyonufaika nao” alisema Mkurugenzi Mtendaji wa TPSF Bwana Francis Nanai

Mgeni rasmi katika Kongamano hilo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mhe. John Mongela ambapo wadau kadhaa wa sekta binafsi wakiwemo wasafirishaji, watoa huduma za fedha, wakulima, wafugaji, wavuvi, kampuni za uzalishaji, viwanda, wakandarasi na wajasiriamali wadogo wadogo walihudhuria kongamano hilo.

Wadau wengine waliohudhuria kongamano hilo ni pamoja na Bodi ya Usajili Wahandisi Nchini, Ofisi ya Usharoba wa Kati, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Bodi ya Usajili Wakandarasi nchini.

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania Ndugu Masanja Kungu Kadogosa amesema kuwa Kongamano hilo ni utekelezaji wa maagizo ya Serikali kuhakikisha sekta binafsi zinashirikishwa katika miradi mikubwa ya kimkakati ili kukidhi makubaliano ya kimkataba katika miradi na kuleta manufaa kwa taifa

Kadogosa aliongeza kuwa “Ujenzi huu wa kipande cha tano ni sehemu ya utekelezaji wa ilani ya Chama Cha Mapinduzi, mradi huu ni mkubwa sana na nina uhakika karibu Trilioni moja itabaki hapa nchini kupitia fursa zitakazopatikana”

Aidha, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TPSF Bi. Angelina Ngalula ameishukuru Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutengeneza fursa kupitia miradi ya kimkakati ukiwemo mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa
“Tunamshukuru Rais Magufuli kwa kutuletea fursa, sisi wadau ni vyema tukajipanga kushiriki wakati wa ujenzi na kuutumia mradi huu utakapokamilika” alisema Bi. Angelina Ngalula

Bi. Ngalula aliongeza kuwa ushirikishwaji wa sekta binafsi katika maendeleo ya nchi ni muhimu kwani hata Mhe. Rais anatambua ushirikishwaji wa sekta binafsi katika maenedeleo na utekelezaji wa miradi ya kimkakati, hivyo wadau wa sekta binafsi wanatakiwa kuyabeba maono ya serikali na kuyafanyia kazi.

Wadau walipata fursa kuuliza maswali na kupata majibu, pia waliweza kutoa maoni juu ya namna ya upatikanaji wa taarifa za fursa za kibiashara katika mradi huo. Kongamano hili linakuwa la kwanza kufanyika nchini kwa lengo la kujadili namna sekta binafsi zitakavyoshiriki katika miradi ya kimkakati nchini.

# WAFANYAKAZI WANAWAKE WA TRC WASHIRIKI SIKU YA WANAWAKE DUNIANI

Na Mwandishi wetu TRC




**KAULI MBIU**
**Wanawake katika Uongozi,**
**Chachu kufikia Dunia yenye Usawa**






Wafanyakazi Wanawake wa Shirika La Reli Tanzania washiriki siku ya Wanawake Duniani inayoadhimishwa kimataifa kila mwaka Machi 8.

Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kitaifa yamefanyika jijini Dar es Salaam katika ukumbi wa Mlimani City ambapo Mgeni Rasmi akiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan huku kauli mbiu ikiwa "Wanawake katika Uongozi, chachu kufikia Dunia yenye Usawa"

Judith George, Mfanyakazi wa Shirika la Reli katika Idara ya Uhasibu ambaye pia ni Mwenyekiti wa Wanawake TRC ameeleza kuwa "Wanawake wa TRC ni miongoni mwa wanawake ambao tunashiriki kila mwaka siku hii, tunamshukuru sana Mkurugenzi Mkuu Ndugu Masanja Kadogosa anatuwezesha kukakimilisha shughuli hii tunamuombea aendelee hivi kila mwaka"

Pia Wanawake wafanyakazi wa TRC wametoa rai kwa wanawake wengine kuchangamkia fursa zilizopo katika mradi wa ujenzi wa Reli ya Kisasa – SGR ili kujikwamua kiuchumi, wameongeza kuwa Shirika linawakaribisha wanawake kutembelea Mradi huo kwani limeweka utaratibu mzuri wa kupata taarifa za mradi huo ikiwemo namna ya kushiriki fursa zilizopo.

Aidha, wanawake hao wamefurahi kushiriki maadhimisho hayo na wanafarijika kwa kuwa kauli mbiu ya mwaka 2021 inaakisi kwa vitendo ushiriki wa wanawake katika uongozi ndani ya Shirika la Reli na wamepongeza wanawake wote waliopo katika uongozi ndani ya Shirika kwa utendaji wao mahiri.

# MATUKIO KATIKA PICHA

Na Mpiga Picha wetu TRC





Aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli akihutubia mara baada ya utilianaji saini mkataba wa ujenzi wa reli ya Kisasa kutoka Mwanza hadi Isaka, Chato mkoani Geita hivi karibuni Januari 2021.



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhandisi Dkt. Leonard Chamuriho akitoa taarifa fupi ya Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa Mwanza - Isaka wakati wa tukio la utilianaji saini mkataba wa ujenzi wa reli hiyo Chato mkoani Geita hivi karibuni Januari 2021.




Aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Magufuli (wa sita kulia) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi mbalimbali wa Serikali ya Tanzania na China mara baada ya kusainiwa mkataba wa ujenzi wa reli ya kisasa Mwanza - Isaka, Chato mkoani Geita hivi karibuni Januari 2021.



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kungu Kadogosa akitoa neno la Shukurani mara baada ya kupokea tuzo ya Kurasa Bora ya Serikali Mtandaoni katika ukumbi wa Akemi jijini Dar es Salaam hivi karibuni Februari 2021.




Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano TRC Bi. Jamila Mbarouk akieleza mikakati inayotumika na Shirika katika kuwasiliana umma katika hafla ya kupokea tuzo ya Kurasa Bora ya Serikali Mtandaoni katika ukumbi wa Akemi jijini Dar es Salaam hivi karibuni Februari 2021.

# MATUKIO KATIKA PICHA

Na Mpiga Picha wetu TRC






Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa akiwa katika picha ya pamoja na Menejimenti ya TRC na Kampuni ya Serengeti Bytes mara baada ya kupokea Tuzo katika ukumbi wa Akemi hivi karibuni, Januari 2021.




Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kungu Kadogosa (kati) akiwa katika picha ya pamoja na Watumishi wa Kitengo cha Habari na Uhusiano TRC mara baada ya kupokea Tuzo ya Kurasa Bora ya Serikali Mtandaoni katika ukumbi wa Akemi hivi karibuni Januari 2021.



Afisa masuala ya jamii kutoka TRC Bi. Lightness Mngulu akiwaelimisha wananchi wa pugu stesheni juu ya kujifunza kupitia mafunzo ya kujikwamua kiuchumi yaliyofanyika mkoani Morogoro hivi karibuni Februari 2021



Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Mhe. Dkt. Leonard Chamuriho akiwa katika picha ya pamoja na Kamati ya Bunge ya Miundombinu na wafanyakazi walioshiriki kukarabati vichwa Sogeza 7 mkoani Morogoro, hivi karibuni Machi, 2021.



Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa akimkabidhi Cheti Muwakilishi wa Kampuni ya Ako Catering Services kutambua mchango wa Kampuni hiyo katika kufanikisha Kongamano la Wadau wa Sekta Binafsi lililofanyika katika ukumbi wa Benki Kuu jijini Mwanza hivi karibuni Januari 2021.




Mkurugenzi Mkuu wa TRC Masanja Kadogosa (wa nne kushoto) akiwa katika picha ya pamoja na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi TPSF Bi. Angelina Ngalula (wa tatu kulia) pamoja na Wajumbe wa Bodi hiyo, Menejimenti na baadhi ya wadau mara baada ya Kongamano la wadau wa sekta binafsi jijini Mwanza hivi karibuni Januari 2021.

# SERIKALI YAZIDI KUTOA HAMASA YA MAENDELEO YA NCHI KWA WANANCHI MKOANI MOROGORO

Na Mwandishi wetu TRC



Maafisa kutoka TRC wakiwahudumia baadhi ya wananchi mkoani Morogoro wakati wa zoezi la ulipaji fidia ili kupisha mradi wa SGR hivi karibuni Februari 2020 hivi karibuni.

Serikali inazidi kutoa hamasa ya kuleta maendeleo ya nchi kwa wananchi wa mkoa wa Morogoro baada ya kuendeleza zoezi la ulipaji wa fidia katika maeneo mbalimbali yaliyobaki ambapo zoezi hilo linafanywa na Shirika la Reli Tanzania ili kupisha ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) kipande cha Dar es Salaam - Morogoro Februari 2021.

Maeneo hayo ni pamoja na maeneo ya kifusi , maeneo yaliyo pitiwa na umeme,maeneo yaliyo ongezeka pamoja na wananchi ambao hawakuwepo wakati wa ufanyaji wa uthamini wa maeneo.

Wananchi mkoani humo wamehamasika katika kufanya maendeleo mbalimbali yatakayoleta faida na mapato ya nchi baada ya kupokea hundi zao.

Licha ya mikakati hiyo ya maendeleo wamefurahishwa sana na zoezi hilo na kuishukuru serikali kutekeleza ahadi ya malipo na kutenda haki kwa wananchi.

Afisa wa masuala ya jamii kutoka TRC Bi. Lightness Mngulu amesema kuwa zoezi linaendelea bila malalamiko ya aina yeyote kutoka kwa wananchi.

“Hadi sasa hatujapata malalamiko ya aina yeyote na endapo likijitokeza tunawapa taratibu za kufuata ili kukamilisha zoezi “ alisema Bi. Lightness.

Wananchi hao wanaokabidhiwa hundi wametoka katika maeneo mbalimbali ya vijijini ikiwemo kijiji cha Mikese, Tanki la maji, Kinonko, Mkambarani, Mtego wa simba, Pangawe pamoja na mtaa wa Yespa.



# WANANCHI JIJINI MWANZA WASHUKURU UJIO WA MRADI WA SGR

Na Mwandishi wetu TRC



Afisa wa Shirika la Reli Tanzania Bwana Paschal Sinyaw (kushoto) akimsainisha mwananchi wa kijiji cha Nyamatala Bwana mikoba M. Mikoba kwa ajili ya kumkabidhi hundi ya malipo ya fidia, Misungwi jijini Mwanza hivi karibuni Machi 2021

Wananchi wa kijiji cha Nyamatala kata ya Ukiliguru wilaya ya Misungwi jijini Mwanza wameishukuru Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujio wa Mradi wa Reli ya Kisasa – SGR jijini humo kufuatia hatua za awali za maandalizi kwa ajili ya mradi huo kuanza, hivi karibuni Machi 2021.

Wananchi wamezungumza hayo walipokuwa wakipokea hundi kwa ajili ya malipo ya fidia ya maeneo yao yaliyotwaliwa kwa ajili ya kituo cha kupakua na kupakia mizigo kwa ajili ya treni za reli ya kisasa kitakachojengwa sambamba na bandari kavu katika eneo la Fela jijini humo.

Wananchi zaidi ya 70 wamekabidhiwa hundi zao katika zoezi lililofanyika kwa siku mbili katika kijiji cha Nyamatala ambapo zaidi ya Shilingi Bilioni 2 zimetumika kwa ajili ya malipo hayo.

Diwani wa Kata ya Ukiliguru Bwana Mathew Makoye ametoa Shukurani kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli kwa kutekeleza ahadi ya kulipa fidia kwa wananchi wa kata hiyo na kuongeza kuwa wananchi wamepokea stahiki zao na wameridhika.

Bwana Mathew alisisitiza kuwa "Mimi na wananchi wangu tumeupokea kwa mikono miwili, kwa sababu mradi huu utakapokamilika utasaidia katika usafiri muda utakaotumika utakuwa ni Saa 6 hadi 7 kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kwahiyo utakuwa na tija kwa wananchi"

Naye mmoja wa wananchi waliopatiwa fidia ili kupisha mradi huo Bwana Lucas Justine ameeleza hisia zake mara baada ya kupatiwa stahiki yake na kusema kuwa "Tumekuja kupatiwa hundi kwa ajili ya malipo ya fidia ya maeneo yetu yaliyochukuliwa kwa ajili ya ujenzi wa SGR, tunapongeza ujio wa reli hii na tutapata fursa za ajira na biashara kupitia mradi huu"

Utekelezaji wa Mradi wa SGR kipande cha 5 Mwanza – Isaka unatarajiwa kuleta fursa za ajira na biashara kwa wananchi hususani wanaoishi kando ya maeneo ambayo mradi huo utakaohusisha ujenzi wa reli yenye urefu wa Kilometa 341, kituo cha Mizigo eneo la Fela na vituo vya reli takribani 7, sambamba na fursa hizo reli itarahisisha usafiri na usafirishaji mizigo kati ya Dar es Salaam na nchi za Uganda na Sudani kusini.




Ujenzi wa Reli ya Kisasa - SGR awamu ya kwanza Dar es Salaam - Mwanza

# TRC YATOA MAFUNZO KWA WANANCHI JUU YA KUJIKWAMUA KIUCHUMI

Na Mwandishi wetu TRC

Shirika la Reli Tanzania - TRC limetoa mafunzo kwa wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa na mradi wa reli ya kisasa - SGR kipande cha kwanza Dar es Salaam - Morogoro kuhusu njia mbalimbali za kujikwamua kiuchumi yaliyofanyika katika ofisi ya kata ya Pugu, eneo la Pugu Stesheni na halmashauri ya wilaya ya Kisarawe Februari 2021.

Mafunzo hayo ambayo yamegawanyika katika makundi tofauti ujasiriamali, ufundi stadi, kilimo cha kisasa na ufugaji pamoja na urasimishaji wa ardhi na hati miliki ambapo yatawasaidia wananchi waliopatiwa malipo yao ya fidia kwa kiasi kikubwa katika kujikwamua kiuchumi.

Afisa wa masuala ya jamii kutoka TRC Bi. Lightness Mngulu ameeleza kuwa lengo la mafunzo hayo ni kutoa mwanga na kuwawezesha wananchi wote waliotwaliwa maeneo kupisha mradi wa SGR kujifunza na kupata elimu ya mambo mbalimbali ya kujiinua kiuchumi.

Bi. Lightness amesema kuwa mafunzo hayo yametolewa na wajuzi mbalimbali wakiwemo afisa kilimo na mifugo, afisa ardhi, wajuzi wa ufundi stadi na wajasiriamali kutoka katika maeneo tofauti ya kata ya Pugu na Wilaya ya Kisarawe. ”Tumewashirikisha watu wenye ujuzi katika nyanja tofauti ili wawe wakufunzi na wananchi waweze kuwapata kwa urahisi” alisema Bi. Lightness.

Vilevile Bi. Lightness amewaasa wananchi kuweka umakini katika kile wanachojifunza na kujitokeza kwa wingi kupata mafunzo hayo ambayo ni muendelezo, ambapo mafunzo hayo hayana gharama yeyote kwa mwananchi.
“Mafunzo haya ni bure na yana faida kubwa kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa wananchi” aliongezea Bi. Lightness.

Kadhalika, mkazi wa eneo la Pugu Stesheni Bi. Pili Salumu ametoa shukrani kwa serikali ya awamu ya tano pamoja na TRC kwa kuandaa mafunzo hayo ambayo yatawasaidia wananchi wengi kujiendeleza na kujiinua kiuchumi.
“Mafunzo ni mazuri sana na yanasaidia mwananchi kutunza pesa na kuwa na umakini na ustadi” alisema Bi. Pili.

Naye fundi chuma katika Halmashauri ya Wilaya ya Kisarawe Bw. Alila Bakari amesema kuwa wamefurahishwa sana na ujio huo wa TRC wilayani humo na kutoa mafunzo kwa wananchi ambayo yatasaidia hadi vizazi vya baadae na vya sasa kuweza kujikwamua kiuchumi na maendeleo.
“Mafunzo haya yana tija kwakua mtu akipata elimu na ujuzi basi atafundisha wengine katika jamii” alisema Bw. Alila.




Mabula Richard Mabula, Mkurugenzi wa Taasisi ya ‘Women and Youth Poverty Alleviation’ akitoa mada wakati wa mafunzo mafunzo ya kujikwamua kiuchumi kwa wananchi, yaliyofanyika katika kata ya Pugu Wilaya ya Ilala hivi karibuni Februari 2021.

# MITANDAO YA KIJAMII NA MAFANIKIO YA MAWASILIANO KWA UMMA SERIKALINI

Na Mwandishi wetu TRC

Mitandao ya kijamii imekuwa nyenzo muhimu ya mawasiliano kwa Taasisi mbalimbali za Serikali, ni njia ya moja kwa moja katika kufikisha ujumbe ama taarifa muhimu kwa wananchi waliokusudiwa. Mfano, uwezo wa kutoa taarifa kwa haraka linapotokea jambo la dharura au ujumbe muhimu kwa wananchi, mitandao ya kijamii imekuwa kinara kwa kufikisha ujumbe kwa haraka na kwa muda sahihi ukilinganisha na njia zingine za mawasilianao kama vile Runinga, Redio na Gazeti.

Kulingana na Ripoti ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania – TCRA (2019) hadi kufikia Desemba 2017 ilionesha kuwa idadi ya watumiaji wa mtandao imeongezeka hadi watu Milioni 23 ambayo ni sawa na 45% ya watanzania wote. Ripoti hii inafichua kuwa matumizi ya mitandao ya kijamii nchini imekuwa ikiongezeka na hivyo kuzifanya Taasisi za Serikani na binafsi kuwekeza mawasiliano yake zaidi katika mitandao ya kijamii lengo likiwa ni kutangaza, kupata wateja, kujulikana na kutunza taswira ambapo itasaidia na imesaidia kampuni mbalimbali na taasisi kukua kibiashara na katika utoaji huduma na hatimaye kukuza uchumi wa nchi.

Shirika la Reli Tanzania – TRC ni miongoni mwa Taasisi za Serikali ambayo kupitia Kitengo cha Habari na Uhusiano wa Umma kimeendelea kutumia mitandao yake ya kijamii katika kufikisha taarifa kwa wananchi ndani na nje ya nchi. Kitengo cha Habari na Uhusiano wa Umma TRC kimekuwa kikitumia mitandao yake ya kijamii Twitter, Facebook, Instagram, LinkedIn kwa jina la @tzrailways pamoja na YouTube kwa jina la TRC Reli TV.

Licha ya kutumia mitandao ya kijamii kama njia ya mawasiliano kati ya Shirika na wadau wake, lakini pia Shirika limefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika kujenga uhusiano mzuri na wananchi kutokana na sera na mpango mkakati mzuri wa mawasliano, ambapo imepelekea Shirika kuibuka kinara wa **KURASA BORA YA SERIKALI MTANDAONI** katika ubunifu na kutoa taarifa kwa umma na zenye kuaminika.

Mapema Februari 16, 2021 Shirika la Reli Tanzania lilipewa tuzo ya Kurasa Bora ya Serikali Mtandaoni iliyopokelewa kwenye hafla fupi iliyoandaliwa na Shirika katika ukumbi wa AKEMI jijini Dar es Salaam. Tuzo hiyo ilipatikana baada ya kushindanishwa katika kipengele cha Kurasa Bora ya Serikali Mtandaoni inayohabarisha wananchi ambapo mashindano hayo yaliratibiwa na kampuni ya Serengeti Bytes kwa kushirikisha mashirika na taasisi zote za serikali na wananchi kupewa nafasi ya kupiga kura na hatimaye TRC iliibuka Mshindi.

Aidha, Katika Hafla hiyo ambayo Mkurugenzi Mkuu wa TRC Ndugu Masanja Kadogosa ambaye alipokea tuzo hiyo alibainisha kuwa tuzo hiyo ni kubwa kwa Shirika na inadhihirisha kuwa kinachofanyika ndani ya Shirika la reli wananchi wengi wanaona kupitia mitandao ya kijamii.

“Sisi tumeona ni jambo kubwa na hata katiba ya Nchi inatambua kuwa vitu vinavyofanyika ndani ya Serikali lazima watu wawe na taarifa, tunatimiza suala la kisheria na vilevile tunatendea haki watanzania wajue pesa yao ya kodi inakwenda wapi” alisema Ndugu Kadogosa.

Sambamba na Tuzo hiyo ambayo Shirika la Reli Tanzania imepata kupitia Kitengo cha Habari na Uhusiano wa Umma, tuangazie mafanikio mbalimbali ambayo Shirika la reli limefanikiwa katika kutumia mitandao yake ya kijamii kwa lengo la kuwasiliana na kufikisha ujumbe kwa hadhira yake na watanzania kwa ujumla. Mafanikio hayo ni kama ifuatavyo.

## Ufanisi katika kuufikia umma

Ni dhana ya kimsingi kwa wataalamu wa mawasiliano, taasisi inapotumia mitandao yake ya kijamii inapanua wigo wa kuifikia hadhira kubwa. TRC imepanua wigo wake katika kuufikia umma na kuongeza wafuasi wake mwaka 2020/21 kutoka 9,638 - 10,638 kwenye kurasa wa Facebook, kutoka 41,400 hadi 44,100 kwenye ukurasa wa Twitter, kutoka 17,064 hadi 18,500 kwenye ukurasa wa Instagram, kutoka 5,944 - 10,470 kwenye ukurasa wa LinkedIn, kutoka kwa Wasajili 50,500 hadi 55,600 kwenye Chaneli ya YouTube.

**Inaendelea Uk. 17**

# MITANDAO YA KIJAMII NA MAFANIKIO YA MAWASILIANO KWA UMMA SERIKALINI

Na Mwandishi wetu TRC

Inatoka Uk. 16




**Kituo cha Ukusanyaji wa Maoni wakati halisi**

Vyombo vya habari vya kijamii ni njia bora ya kusambaza habari kwa haraka na vile vile kutoa nafasi ya kuweka maoni na kupokea maoni hayo. TRC imeendelea Kukusanya taarifa kutoka kwa wafuasi wake ambapo maoni hayo yameweza kukusanywa na kuchambuliwa kwa lengo la kutoa ufafanuzi katika suala lililoibuka lakini pia maoni hayo ya wadau hutumika katika kuboresha huduma na utendaji kazi.

**Kubadilisha Mtazamo wa Umma na kuongeza ufahamu wa kazi na malengo ya Shirika**

Mitandao ya kijamii hutumika katika kubadili mitazamo mbalimbali ya umaa kuhusiana na Shirika katika mambo kadha wa kadha. Mitandao ya kijamii hutoa fursa ya kujua dhamira ya shirika ni nini na hata mipango ya sasa ni nini, TRC kwa kutumia mitandao yake ya kijamii imeongeza uelewa kwa umma kwa kutoa taarifa nyingi na mipango yake ijayo. Hivyo basi wataalamu wa masuala mawasiliano ya umma wanaweza kusaidia kubadilisha mtazamo wa umma na taasisi za Serikali.

**Usambazaji wa Taarifa kwa gharama nafuu.**

Vyombo vya habari vya kijamii ni kituo cha usambazaji bora na cha gharama nafuu. Ifahamike kuwa baadhi ya mitandao ya kijamii haihitaji pesa nyingi au haihitaji kabisa pesa katika kusambaza ujumbe. Ni muhimu sana kwa Taasisi za Serikali kutumia vyombo vya habari vya kijamii, kwani uwekezaji wake ni wa nafuu lakini matokeo yake ni ya faida kubwa kwa masirahi ya umma.

**Njia bora ya kuchanganua matokeo**

Mitandao ya kijamii hutoa nafasi kwa wafuasi kutoa maoni yao kuhusu taarifa iliyotolewa na taasisi husika. TRC kupitia mitandao ya kijamii imesaidia kupata ufahamu wa wakati halisi juu ya habari gani wananchi wake wanapendezwa nayo, wapi na kwenye mtandao gani wa kijamii. Kwa kupitia mitandao hiyo shirika lina uwezekano wa kutumia habari hiyo kuchanganua matokeo maoni ya kile ambacho kimeongelewa kwa masirahi ya umma na shirika

**Kuwepo kwa Uwazi**

Uwazi ni moja ya nguzo muhimu katika taasisi ya umma pia uwazi unathaminiwa na umma wa watanzania, ingawa kuna sheria ambazo zimetilia mkazo juu ya uwazi katika mawasiliano yote ya serikali. Katika mambo ambayo yanagusa umma na yenye maslahi kwa nchi, TRC imeendelea kutoa habari kwa umma kuhusu miradi mikubwa inayosimamiwa na Shirika ambayo ni Reli ya kisasa – SGR, mradi wa uboreshaji wa reli ya kisasa – TIRP, ukarabati wa Behewa sambamba na huduma zinazotolewa na Shirika. Kwa kutoa taarifa hizo imekuwa ni njia bora ya kupata uaminifu kwa umma na uaminifu huo umelijengea heshima shirika kuwa kituo cha utoaji taarifa ambazo ni sahihi na za kuaminika.

Walakini, licha ya faida zilizo wazi zinazohusiana na mitandao ya kijamii, mashirika mengi ya serikali bado yanajitahidi kuongeza jitihada katika matumizi ya mitandao ya kijamii. Kwa kuzingatia ukuaji wa Teknolojia na umuhimu wa mitandao ya kijamii, kuna maeneo muhimu ambayo mashirika ya Serikali yangeona faida zinazoweza kutokea katika mawasiliano endapo wataongeza juhudi katika kutumia mitandao ya kijamii kama njia mojawapo ya kufikisha ujumbe kwa hadhira.

# AFYA NA HAKI ZA MFANYAKAZI BAADA YA KUUMIA KAZINI

Na Mwandishi wetu TRC

Kumekuwa na upungufu wa elimu juu ya watu ambao kwa bahati mbaya wanaumia wakitekeleza majukumu yao na kushindwa kuelewa haki zao na utaratibu wa kuzipataka, ambazo kwa mujibu wa sheria wanstahili kuzipata, Kwa kushindwa kupata maarifa sahihi juu ya mambo haya kunapelekea watumishi kulaumu wasiohusika, kwani baadhi yao hulaumu kampuni, maafisa rasilimaliwatu, wakili na mwanasheria na hata wengine hulaumu kitengo cha afya.

Leo tutatoa maarifa yatakayomsaidia yeye na wengine ambao yamkini hawajajua nini cha kufanya pindi wanapopata matatizo ya kiafya wakiwa kazini.

Tuanze kwa kujua makundi haya matatu ya magonjwa, mosi kuna magonjwa ya kawaida, pili kuna magonjwa yanayotokana na kufanya kazi fulani na tatu ni ajali mbalimbali.

Ajali zote ziwe za kawaida au za gari zina utaratibu. Tukianza na magonjwa ya kawaida kama Malaria na Homa za matumbo, haya yakisharipotiwa katika kliniki, wagonjwa huruhusiwa kwenda kutibiwa katika Zahanati, vituo vya afya na hata hospitali za serikali za karibu.

Magonjwa haya ya kawaida huwa hayana fidia, kwa upande mwingine Magonjwa yanayotokana na kazi au ajali zinazotokea wakati wa kufanya kazi ambapo hulipwa fidia na yana utaratibu ufuatao; Wataalamu wa afya watamchunguza, kisha mgonjwa atapatiwa maelezo ya kina ni jinsi gani kazi yake imepelekea yeye kupata madhara au ugonjwa na kumshauri endapo watabaini kuwa ugonjwa huo unatokana na kazi.

Endapo utahitajika ushauri na matibabu ya kitaalamu zaidi madaktari humshauri mgonjwa na hata kuratibu rufaa yake. Mgonjwa akishamaliza matibabu/ufuatiliaji wa afya yake na

## KUMBUKA

**“Magonjwa yanayotokana na kazi au ajali zinazotokea wakati wa kazi hulipwa fidia”**



tathmini ya uzito wa tatizo lake, watoa huduma za afya hujaza fomu maalumu kwenda kwenye mamlaka husika ya kutoa fidia kwa wafanya kazi (WCF).

Baada ya kujaziwa fomu hizo hupelekwa kwa madaktari walioteuliwa kuthibitisha magonjwa hayo na namna matibabu yalivyofanyika na hatimaye mfanyakazi hupata stahiki zake kulingana na kima cha mshahara aliokuwa akiupata mpaka anapatwa na ugonjwa huo pamoja na kipindi cha kuchangia katika mfuko huo.

Kwa upande wa ajali na hasa tukijikita katika ajali za magari ni lazima Polisi fomu namba 3, 90, 115 na hiyo ripoti kamili kutoka mfuko wa walipa fidia za wafanyakazi zijazwe.

Polisi ni lazima waandae ripoti baada ya kupima ajali na kuelezea chanzo cha ajali, watu wa usalama kazini ni lazima pia wawe na maelezo katika ripoti yao pamoja, pia mtoa huduma ya afya lazima atoe ripoti ni kwa namna gani aliweza kumpokea majeruhi, huduma gani aliitoa na kumpeleka kwa gari za dharula ili akapatiwe matibabu katika vituo vikubwa vya afya (kama ilihitajika).

Viongozi wa vyama vya wafanyakazi, idara ya rasilimali watu, idara ya afya na usalama mahala pa kazi na kamati ya afya na usalama kazini ni miongoni mwa idara/vitengo vinavyotakiwa kuufahamu utaratibu huu, kwani wao ndio waelimishaji wakuu katika masuala yahusuyo haki na wajibu wa mfanyakazi.

Mwisho tunapaswa kuzijua sheria zenye kuelezea haki za wafanyakazi (workers compensation act), pamoja na hayo yote tunawajibika kutoa elimu ya afya yenye kuwafanya wafanyakazi kuwa salama na kuweza wa kujikinga na maambukizi ya magonjwa ya mlipuko kama Covid19, Kifua Kikuu, Tauni na Kipindupindu na magonjwa mengine ikiwemo VVU/UKIMWI.




**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**
**Barabara ya Sokoine**
**S.L.P 76959**
**Dar es Salaam**
**TANZANIA**
**Barua pepe; info@trc.co.tz**
**Simu ya Bure; 0800 110 042**



Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
**SHIRIKA LA RELI TANZANIA**

| | |
|---|---|
| **MHARIRI MKUU** | **Jamila Mbarouk** |
| **MHARIRI MSAIDIZI** | **Sami Omary** |
| **MAKALA** | **Aziza Charles & Hemed Mohamed** |
| **HABARI** | **Amina Juma** |
| **PICHA** | **Seleman Kadiko** |
| **KIBONZO** | **Hassan Said** |
| **MTAYARISHAJI** | **Sami Omary** |


**tzrailways** **TRC Reli TV** **www.trc.co.tz**

**Reli Yetu | Maendeleo Yetu | Taifa Letu #TRCMpya**